# VIKUNDI & USHIRIKA

MRADI ULIYOFANYWA NA CCCEP | MUHTASARI NAMBA 4 | SEPTEMBA 2024

Kuelewa vichocheo na vikwazo vinavyoathiri uanachama na ushiriki katika vikundi vya kijamii ni muhimu sana kwa uundaji na utekelezaji wa sera za maendeleo. Chuo Kikuu cha Leeds kimekuwa kikifanya utafiti kwa karibu miaka kumi kuhusu jinsi jamii zinazoshi katika Milima ya Usambara Mashariki kaskazini-mashariki mwa Tanzania zinavyopata uzoefu wa vikundi na ushirika kupitia mradi wa GCRF-AFRICAP pamoja na tafiti za Shahada za Uzamivu.

Hivi karibuni, FoSTA-Health imekuwa ikifanya tafiti juu uanzishwaji na uendeshaji wa vikundi, pamoja na fursa na changamoto za uanachama. Utafiti huu pia unahusisha jinsi maarifa na manufaa yanayotokana na vikundi na ushirika yanavyonufaisha jamii kwa ujumla wake. Nakala hii fupi inatoa muhtasari wa baadhi ya matokeo yetu muhimu kuhusu kipi kinafaa na kipi hakifaa katika uanzishwaji na uendeshaji wa vikundi na ushirika.



## UANZISHWAJI WA VIKUNDI

### VIGEZO VYA UTEUZI

Ukosefu wa rasilimali za kutosha unaweza kupunguza idadi ya wanachama wa vikundi, huku vikundi mbalimbali vikitumia vigezo tofauti katika uteuzi wa wanachama. Hali hii mara nyingi husababisha mkanganyiko kuhusu vigezo vya uteuzi, ambapo mara nyingine kunaweza kuibuka mitazamo ya upendeleo, hasa kuhusu nani anayeonekana kuwa mchapakazi au anayependwa zaidi. Changamoto hizi zinaweza kuathiri utendaji wa vikundi (kwa mfano, utekelezaji wa faini na kufuata sheria ndogo) na pia kudhoofisha mahusiano ya kijamii kwa upana zaidi (kama vile kuzua shaka na kupoteza imani na uongozi).

Ni muhimu kuhakikisha kwamba taarifa na hatua za uanzishaji zinawafikia wanajamii wote – hasa wale walio katika mazingira magumu na waliotengwa. Aina mbalimbali za uhamasishaji zinapaswa kutumika, kwa mfano, zaidi ya kuwasilisha taarifa katika mikutano mikuu ya vijiji ambako si kila mtu anahudhuria. Hii itasaidia kuwafahamisha wananchi wote kuhusu uanzishwaji wa vikundi na kufanya vigezo na taratibu za uteuzi kuwa wazi zaidi.

### MAHITAJI YA UANACHAMA

Katika wilaya ya Muheza iliyopo Milima ya Usambara Mashariki, wanaume hushiriki zaidi katika vikundi ukilinganisha na wanawake. Hii inaweza kuwa kwa sababu mbalimbali, kama vile wanawake mara nyingi wana majukumu ya nyumbani zaidi kuliko wanaume, jambo linalomaanisha kuwa wanakuwa na muda mdogo wa kushiriki katika kazi za vikundi. Pia, wanaweza kutoruhusiwa kujiunga na vikundi na waume zao, au labda hawaoni sababu ya kujiunga ikiwa mume tayari ni mwanachama. Hata hivyo, wale wasiokuwa wanachama wa vikundi mara chache wanapata manufaa ya vikundi, kama vile mafunzo na elimu. Baadhi ya vikundi pia vina masharti ya kifedha ambayo si kila mtu anaweza kumudu. Hali hii inapunguza idadi ya watu wanaoweza kujiunga.

Hivyo basi, ni muhimu kuzingatia jinsi ya kuhakikisha kwamba wanajamii wote wanapata fursa ya kujiunga na vikundi, iwapo watataka. Hii inaweza kujumuisha msaada wa ziada kwa wanawake, kama vile huduma za uangalizi wa watoto au msaada wa kifedha, ambao unaweza kuwapa muda na rasilimali za kutosha ili waweze kuwa wanachama.

### MTIZAMO WA JAMII

Vikundi ni njia rahisi kwa mashirika ya maendeleo na sera kufikia idadi kubwa ya watu. Hata hivyo, si kila mtu anataka kuwa katika kikundi. Wakulima wengine wanapendelea kufanya kazi nje ya vikundi. Mbinu za maendeleo zinahitaji kutambua hili na kuwatambua wakulima hawa kwa kutoa nafasi kwao katika mipango yao ya maendeleo.

Moja ya sababu kuu za kutotaka kujiunga na vikundi ni kutokana na historia ya ushirika na vikundi vya nyuma.

Baadhi ya vikundi na ushirika vilishindwa au kuvunjika kutokana na usimamizi mbovu wa kifedha, wanachama wasio waaminifu, na ahadi zisizotekelezwa kutoka kwa mashirika ya maendeleo na watunga sera. Ni muhimu kutambua jinsi miradi ya hapo awali ilivyoathiri mitazamo ya sasa kuhusu vikundi, ushirika, na kiwango cha imani kwa taasisi. Watendaji wanapaswa kusikiliza na kujumuisha maoni ya jamii kuhusu kipi kinafaa na kipi hakifai.

## UTENDAJI KAZI WA VIKUNDI

### MUUNDO

Wakati mwingine kuna mgongano au kutokulandana kati ya malengo na madhumuni ya vikundi na yale ya watendaji wa maendeleo. Hali hii mara nyingi huathiri kwa kiasi kikubwa utendaji na uendelevu wa vikundi baada ya kipindi cha utekelezaji wa mradi kumalizika. Ni muhimu kuwa wazi tangu mwanzo ili kusimamia matarajio na kuepuka kutoa ahadi kubwa kupita kiasi, jambo ambalo linaweza kusaidia kuhakikisha kufuatwa kwa taratibu za kisheria.

Njia moja ya kufanikisha hili ni kuhakikisha ushirikishwaji wa jamii tangu hatua za awali za mchakato. Hii inajumuisha kufanya kazi pamoja na jamii kwa kusikiliza, kuelewa, na kujumuisha matamanio, matarajio, na changamoto zao katika muundo wa vikundi. Uongozi na majukumu yanapaswa kuwa ya wazi na yenye uwazi, pamoja na kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu maendeleo ya vikundi.

### SHUGHULI NA TAARIFA

Mara nyingi wanachama wa vikundi hulalamikia ushiriki duni katika shughuli za vikundi. Hali hii inaweza kusababisha kasi kubwa ya kujiotoa kwenye kikundi na hata migogoro. Kawaida, ni wanachama maskini, walio katika mazingira magumu, na waliotengwa zaidi ambao hukumbana na changamoto za kushiriki shughuli hizo – hasa wale wenye majukumu ya malezi.

Aidha, uwezo wa kupokea na kuchakata taarifa nyingi kwa muda mfupi hutofautiana kati ya mtu na mtu, jambo linaloweza kusababisha mzigo wa taarifa na kupelekea baadhi yao kujiondoa.

Inahitajika juhudi za ziada kuhakikisha kwamba taarifa na shughuli zinazingatia uwezo wa mwanakikundi kuzipokea na kufanyia kazi . Vilevile, ni muhimu kuzingatia kalenda za msimu na shughuli za maisha ya kila siku za wanajamii dhidi ya mahitaji ya muda wa miradi. Hii itasaidia kuleta uwiano kati ya shughuli za miradi na maisha ya wanajamii, hivyo kuongeza ushiriki na uendelevu.

### UTATUZI WA MIGOGORO

Migogoro inaweza kuwa ya kawaida katika vikundi pale ambapo kuna kutofautiana kwa matarajio na uwezo wa kushiriki. Kwa mfano, pale ambapo majukumu ya uongozi na shughuli za vikundi hazijawekwa wazi, inaweza kusababisha kutoelewana kuhusu usimamizi wa fedha ndani ya vikundi. Utamaduni wa kulaumiana ndani ya jamii unaweza kuathiri mahusiano ndani ya vikundi na pia uhusiano mpana wa kijamii.

Ni muhimu kuandaa mafunzo jumuishi juu ya utatuzi wa migogoro ndani ya vikundi, pamoja na kuhamasisha ufahamu kwamba adhabu na faini siyo mara zote mbinu bora za kusimamia migogoro. Kujumuisha mila na desturi za kijamii za upatanisho kunaweza kusaidia kuimarisha mshikamano na kuleta suluhisho endelevu.

## FURSA

Kuwaleta watu pamoja kushirikishana mawazo na kufanya kazi kwa pamoja kunaweza kusaidia kujenga uwezo wa pamoja wa jamii (tazama muhtasari namba 3). Hatua za pamoja na ushirikiano zinaweza kuimarisha uwezeshaji kwa kusisitiza mshikamano, kufanya kazi kwa pamoja, na msaada wa pande zote ili kufanikisha malengo ya pamoja.

Kazi za vikundi pia hutoa msingi wa kujaribu mbinu bunifu zaidi za ushirikishwaji (tazama muhtasari namba 5) ili ziweze kuwa jumuishi zaidi kwa maskini na walio katika mazingira magumu.

Ni muhimu kuzingatia urithi wa vikundi vya zamani – kwa kujifunza kutoka kwa kile kilichofanya kazi vizuri na kujenga juu ya mafanikio hayo. Mitazamo ya jamii inapaswa kuwa sehemu kuu ya mchakato huu wa tafakari na kujifunza – kwani jamii ina mitazamo na uzoefu wa kipekee.

## CHANGAMOTO

Moja ya changamoto kuu ni kuhusu ugawanyaji wa manufaa yatokanayo na vikundi – manufaa kama mafunzo, elimu na fedha. Vikundi vingi vinatumia walimu wa ngaazi ya jamii (CBTs) kwa kudhani kwamba CBTs hawa wanatoa elimu kwenye vikundi na nje ya vikundi. Hii siyo kila wakati inatokea, hasa ikiwa hakuna motisha kwa CBTs kufanya hivyo, na inaweza kusababisha wale wenye nguvu ya kifehda au uelewa wakate mfumo huu wa vikundi na manufaa haya yakaenda kwa vikundi vichache au watu wachache.

Inahitajika kuzingatia kwa umakini mbinu za kuepuka "mzigo wa ushiriki," ambapo muda unaohitajika kwa kazi za vikundi unazidi manufaa yanayotokana na ushiriki huo. Ni muhimu kuepuka watu wachache wenye uelewa Zaidi kwenye jamii kuteka vikundi, zingatia kutoa msaada unaofaa ili kuwezesha walio katika mazingira magumu kushiriki kikamilifu, kama vile watu wenye ulemavu, wazee, watoto, na wale wanaokutana na changamoto za kudumisha uanachama wao.

Changamoto nyingine muhimu ni uendelevu wa vikundi baada ya kumalizika kwa kipindi cha mradi. Ushirikishwaji wa kijamii kupitia udhibiti wa raia (tazama muhtasari namba 5) utasaidia kuhakikisha uhai wa vikundi.

## MAPENDEKEZO

- Hakikisha kwamba taarifa kuhusu uanzishwaji wa vikundi vipya na vigezo vya uteuzi wa wanachama kunakuwa na ushirikishwaji kwa upana na kwa njia mbalimbali ili kila mtu apate taarifa muhimu za kujiunga iwapo atapenda.
- Zingatia ni msaada gani wa ziada (ikiwa upo) unaweza kutolewa ili kuwezesha walio katika mazingira magumu kushiriki kikamilifu – hii inaweza kuwa msaada wa kifedha au msaada wa uangalizi wa watoto ili kutoa muda kwa wanawake.
- Kuwa na mikutano mara kwa mara na jamii ili kujadili masuala yanayowezekana na yasiyowezekana katika uanzishaji na uendeshaji wa vikundi, na jumuisha mitazamo yao katika kazi yako.
- Jumuisha a) mafunzo ya utatuzi wa migogoro, na b) mfumo wa uendelevu baada ya kumalizika kwa mradi katika shughuli za vikundi.

Prepared and disseminated through collaboration with the ESRC Climate Change Centre for Economics and Policy Legacy project led by UoLeeds and Tanzania Forest Conservation Group

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Centre for Climate Change Economics and Policy
An ESRC Research Centre

To find out more about the project, please visit fosta-health.eu

FOSTA HEALTH